BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 26 Septemba, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Ripoti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi juu ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

III. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

102. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Ni ipi kauli na mikakati ya Serikali katika kuwahakikishia wananchi kwamba nchi inakuwa salama kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2025.

**Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

173. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

(a) Kuna athari gani za kiafya na kimazingira zinazotokana na pampasi katika mazingira tunayoishi.

(b) Kwa asilimia ngapi Serikali imefanikiwa kutokomeza madhara ya pampasi mpaka sasa.

**Ofisi ya Rais, Ikulu:**

164. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

(a) Ziara ngapi zenye mnasaba na mashirikiano na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi, zimefanyika katika mataifa mbali mbali kwa miaka mitatu iliyopita.

(b) Je, ni ziara ngapi zimefanywa na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kuja Zanzibar kwa mnasaba huo huo wa kukuza mahusiano mema.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

94. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kuna tofauti gani iliyopo katika masharti ya kupata mikopo ya Serikali kwa vikundi vya wajasiriamali na masharti yanayotolewa na mikopo ya kausha damu ikiwemo BRACO.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

257. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ili kutoa haki katika suala la ununuzi ni wajibu kwa Serikali kuanzisha chombo cha rufaa kinachohusiana na masuala ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma.

Ni chombo gani Zanzibar kinachofanya kazi hiyo.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

119. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Ni lini jitihada za wananchi wa jimbo la Mwanakwerekwe za kuyaondoa majaa karibu na makaazi ya watu zitaungwa mkono na Serikali.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

97. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni utaratibu gani unaotumika kuhakikisha kwamba wanafunzi waliosoma kwa mkopo wa Serikali wanarudisha mikopo yao kwa namna inavyostahiki.

267. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi kubwa ya kuongeza miundombinu ya skuli za kisasa kwa Unguja na Pemba. Pamoja na jitihada hizi, lipo jambo moja ambalo limekuwa na malalamiko makubwa kwa wadau na walimu wa michezo kwamba skuli hizi nyingi zinakosa maeneo ya michezo kwa watoto kama vile viwanja vya mpira.

(a) Serikali inachukua hatua zipi kulitatua tatizo hili.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maeneo ya michezo kwa skuli zetu ili kuongeza fursa ya vijana kuingia katika michezo.

(c) Kwa nini Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka wa kuanzisha skuli za michezo ambazo zitaongeza ari ya vijana kwenye eneo hili.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

26. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Nane ina dhamira kubwa ya kuwainua kimaendeleo vijana wake.

Ni upi mpango wa Serikali wa kuwarasimisha vijana wenye ujuzi mbali mbali ambao kwa sasa hawatambuliki rasmi.

114. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Vijana wanahitaji miradi ya kimkakati itakayowainua kiuchumi na kimaendeo.

Ni miradi ipi inayotarajiwa kuwawezesha vijana kuzalisha mnyororo wa ajira za kujitegemea ili iweze kuwa endelevu kwa manufaa ya vijana wengine.

**Wizara ya Afya:**

39. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa juhudi zake mbali mbali inazozichukua ili wananchi wake waweze kupata huduma bora za afya. Hata hivyo, baadhi ya vituo vya afya bado hali zake haziridhishi na kupelekea kupungua ufanisi wa kazi na kupatikana huduma bora vituoni hapo.

Je, ni upi mpango wa Serikali wa kukifanyia ukarabati kituo cha afya cha Kibondeni kwa dhamira ya kukuza ufanisi wa kazi na kupatikana huduma bora.

40. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ililazimika kuvunja kituo cha afya cha Mvumoni ili kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba.

Ni upi mpango wa sasa wa Serikali wa kujenga kituo chengine cha afya ili wananchi wa eneo hilo na eneo la karibu waweze kuendelea kupata huduma hiyo bila ya usumbufu wowote.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

33. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Miongoni mwa bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vilivyopo Zanzibar ni sukari. Bidhaa hii ni moja kati ya bidhaa muhimu kwa wananchi wa Zanzibar.

Ni upi uwiano wa sukari inayozalishwa hapa Zanzibar na inayotokea nje ya Zanzibar.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**26 Septemba, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**